**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

HALMASHAURI YA WILAYA YA KILINDI

SHULE YA SEKONDARI KIKUNDE
S.L.P 69
SONDE-KILINDI
10/12/2020.

Kumb Na: KKSS/FR-1/2020.

JINA LA MWANAFUNZI____________________________________________

C/O MZAZI/MLEZI ________________________________________________

S.L.P 18
SONGE-KILINDI.

**YAH:MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIKUNDE WILAYA YA KILINDI**

**MKOA WA TANGA MWAKA 2021.**

Ninayo furaha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Kikunde mwaka 2021. Mhula wa kwanza utaanza tarehe 11/01/2021 na wewe unatakiwa kuripoti shuleni hapa tarehe 11/01/2021. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 25/01/2021.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

1. SARE ZA SHULE – wasiliana na uongozi wa shule 0782 780 055 au 0687 207 777
   A. WAVULANA
      1. Suruali ya kijani yenye mifuko mitatu, jozi/pea mbili na isiwe (modo) ya kubana miguu kama mdomo wa chupa na isiwe inaishia makalioni tutakukagua kuhakikisha viwango vya ubora wa suruali hizo.
      2. Shati jeupe lenye mikono mifupi jozi mbili.
      3. T-shirt yenye rangi ya bluu iliyoiva round cover.
      4. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi na gidamu jozi mbili.
      5. Sweta la bluu iliyoiva (dark bluu) coler ya V shape.
      6. Soksi nyeusi jozi mbili.
      7. Raba za michezo.
      8. Bukta na T-shirt za michezo.
      9. Mkanda mweusi wa kawaida usio na bakoli ya kihuni.

   B. WASICHANA
      1. Sketi ya rangi ya kijani malinda ya boksi jozi mbili ivuke goti na kuishia karibu na kifundo cha mguu.
      2. Shati jeupe lenye mikono mifupi jozi mbili.
      3. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na gidamu vyenye visigino vifupi jozi mbili na sio bajaji.
      4. Sweta la bluu iliyoiva coler ya V shape na T-shirt mbili za bluu iliyoiva round coler.
      5. Soksi nyeupe jozi mbili.
      6. Raba za michezo.
2. ZANA ZA KAZI
   A. Daftari kubwa kumi (Counter Book 3 Quire)
   B. Kalamu mbili za wino bluu au nyeusi, penseli na rula
   C. Mkebe wa vifaa vya hisabati (Mathematical set)
3. VIFAA VYA USAFI
   A. Kwanja moja, jembe na panga (vipya).
   B. Ndoo ndogo moja (mpya yenye mfuniko).
   C. Fagio la chelewa.

4. CHAKULA

Kama waraka na mwongozo wa serikali unavyoonyesha juu ya elimu bure kwenye kipengele cha nne (c) ambacho kinasomeka kuwa majukumu ya mzazi/mlezi ni kuhakikisha kuwa huduma zifuatazo zinapatikana kwa mwanafunzi.

A. Sare za shule na michezo kwa wavulana na wasichana track za bluu.
B. Vifaa vya kujifunzia vikiwemo daftari na kalamu.
C. Chakula kwa wanafunzi wa kutwa.
D. Matibabu.
E. Nauli ya kwenda na kurudi shuleni kwa wanaotumia usafiri na walioko shule za sekondari za bweni wakati wa likizo.
F. Mahitaji mengine ya kibinadamu kwa wasichana na wavulana kama vile magodoro,mto na shuka hivyo kila mzazi anatakiwa kuchangia chakula kama ilivyoafikiwa kwenye kikao cha wazazi, bodi ya shule na kata kama ifuatavyo;-
   1. Mahindi debe moja (kg 20)
   2. Maharage kg 5

   Mahitaji hayo unatakiwa kuyawasilisha kwenye kamati ya CHAKULA iliyoundwa na wazazi kabla ya tarehe 25/1/2021.

5. MAADILI

A. HESHIMA: Waheshimu walimu, wafanyakazi, wananchi na wanafunzi wenzako ndani na nje ya shule.
B. SHERIA ZA NCHI: Wajibu wa kila mwanafunzi kuheshimu bendera ya Taifa, picha za viongozi wa taifa, wimbo wa taifa, fedha ya taifa na nembo ya taifa.
C. USAFI: Usafi wa mwili na mavazi ni muhimu hapa shuleni na nje ya shule.
D. MASOMO: Kila mwanafunzi anatakiwa kufuata ratiba ya shule kama ilivyopangwa. Mwanafunzi anatakiwa kuwahi shuleni na kubaki shule hadi mwisho wa shughuli za siku. Mwanafunzi ataondoka shuleni kwa ruhusa.

6. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUSIMAMISHWA AU KUFUKUZWA SHULE.

A. Wizi
B. Uasherati, Ushoga na ubakaji.
C. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi, cocaine
D. Kupiga au kupigana.
E. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
F. Kudharau Bendera ya Taifa.
G. Kuwa mjamzito au kusababisha ujauzito (mimba).
H. Kuoa au kuolewa.
I. Kutoa mimba.
J. Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
K. Kugoma au kukataa adhabu kwa makusudi.
L. Kuwa na simu ya mkononi.

MUHIMU: 1.Kwa wasichana wote toka Malali, Mafulila, Chang'ombe, Seita na Matanda wanatakiwa kuishi bwenini.

2.Fomu namba tatu ijazwe na daktari baada ya vipimo na irudishwe shuleni wakati wa kuripoti.

KARIBU SANA KIKUNDE SEKONDARI

MUSSA M . MSAMI
MKUU WA SHULE

HEADMASTER
KIKUNDE SECONDARY SCHOOL

KILINDI DISTRICT COUNCIL – KIKUNDE SECONDARY SCHOOL

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

From The Head of School

Kikunde Secondary School

P.O Box 69

Songe –Kilindi

10/12/2020.

To Medical Officer________________________________

________________________________________________

Part A:

Please examine the above named student as to his/her physical and mental fitness for a full time student. The examination should be as indicated in part B below.

In each category or sub-category of which will render the application in-eligible in case of a defect pregnant (category iv) will also render a girl student ineligible for studies.

Date____________________________ Signature ______________________________

Part B: MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a Government Medical Officer)

I have examined the above named student and consider that he/she is physically fit/unfit for a full time student.

(i) A. Eye sight ______________________________________________

B. Hearing ______________________________________________

C. Speech ______________________________________________

D. Limbs ______________________________________________

E. Venereal Diseases ______________________________________

F. Leprosy ______________________________________________

(ii) Neuroses ______________________________________________

(iii)Other Serious Diseases ______________________________________

(iv) Pregnancy ______________________________________________

Station _______________Signature _______________Date_____________Designation__________